

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

Anuani ya Simu: "UTUMISHI" D.S.M

Simu Na: +255 22 2118531/4
Nukushi: +255 22 2125299
Barua Pepe: ps@utumishi.go.tz
Tovuti: www.utumishi.go.tz



Menejimenti ya Utumishi wa Umma
na Utawala Bora,
Jengo la Utumishi,
8 Barabara ya Kivukoni,
S. L. P. 2483,
11404 DAR ES SALAAM.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU MADAI YA WALIMU

Gazeti la **Habari Leo** la tarehe 18 Januari, 2017 lilichapisha habari yenye Kichwa cha Habari "**Walimu waitaka Serikali ilipe malimbikizo ya Shilingi Trilioni 1,060/=**." Taarifa hiyo ilimnukuu Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) Bw. Ezekiel T. Oluoch. Aidha, magazeti ya Nipashe na Tanzania Daima ya tarehe 08 Februari, 2017 yamechapisha habari yenye vichwa vya habari "**Walimu watangaza mgomo nchi nzima**" na "**Walimu waitisha Serikali**" yakimnukuu Rais wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Bw. Gratian Mukoba kuwa iwapo Serikali haitalipa madai ya Walimu kiasi cha shilingi bilioni 800/= hadi Machi mosi mwaka huu watatangaza mgomo nchi nzima.

Serikali inapenda kutoa ufafanuzi kuwa kuanzia mwaka 2013/14 hadi sasa imepokea madai ya watumishi wa umma wakiwemo Walimu. Madai hayo yamegawanyika katika makundi mawili kama ifuatavyo:-

1. **Madeni yanayotokana na Mshahara:-** Haya ni madai ya watumishi yanayotokana na kutorekebishiwa mishahara baada ya kupandishwa vyeo, ajira mpya, kumalizika kwa mashauri ya nidhamu na kuteuliwa katika vyeo vya Madaraka. Madai haya hulipwa kwa kutumia Bajeti ya Mshahara. Takwimu zilizopo zinaonesha kwamba kuanzia mwaka 2013/14 hadi 2015/16 Serikali ililipa madeni ya walimu yanayotokana na mishahara kama ifuatavyo:-

Mwaka 2013/14 Serikali ililipa madai ya walimu 31,878 ya **Shilingi 23,730,328,420.65** kati ya madai ya watumishi wote 53,852 yenye jumla ya **Shilingi 47,768,552,199.24**.

Mwaka 2014/15 Serikali ililipa madai ya walimu 35,545 ya **Shilingi**

